JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

MKUU WA TAKUKURU MKOA
Mtaa wa Uzunguni,
S.L.P 37,
37101 SHINYANGA,
Tanzania.
Simu: (028) 2762630
Nukushi: (028) 2763358

22 JULAI, 2020.

TAARIFA KWA UMMA.

TAKUKURU SHINYANGA YAREJESHA MILIONI 41.2 ZA WASTAAFU WALIOATHIRIKA NA MIKOPO UMIZA MKOANI SHINYANGA.

Hii ni taarifa ya kazi zilizofanywa na TAKUKURU mkoa wa Shinyanga katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2019/2020 (Aprili-Juni 2020).

Pamoja na kazi nyingine za kawaida za TAKUKURU ikiwemo Uchunguzi, Elimu kwa umma, Kuzuia Rushwa, Ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuendesha kesi zilizofunguliwa mahakamani kwa makosa mbalimbali ya Rushwa, TAKUKURU mkoa wa SHINYANGA ilifanya ufuatilia wa mikopo umiza kwa wastaafu wa Mkoa wa Shinyanga.

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2020 TAKUKURU mkoa wa Shinyanga iliweza kurejesha kiasi cha jumla ya shilingi **41,268,000/=** kati ya shilingi **110,618,000/=** za wastaafu watano (5) walioathirika na mikopo umiza mkoani Shinyanga kutoka kwa wakopeshaji mbalimbali. Wastaafu hao waliorejeshewa fedha ni kama ifuatavyo:-

1. Mstaafu wa kwanza:
Huyu ni mwalimu mstaafu, aliyekopa kiasi cha Tshs. 7,000,000/= kutoka kwa watu watatu tofauti ikiwemo kampuni moja iliyopo Manispaa ya Shinyanga kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo baada ya kupata mafao ya kustaafu.

Baada ya mafao yake kutoka mnamo tarehe 06/05/2017 wakopeshaji walimlazimisha kulipa fedha kama ifutavyo:-

Mtuhumiwa wa kwanza akiwa mtumishi wa kampuni ya ukopeshaji ya **MALICHA MICROCREDIT CO LTD** yeye binafsi alimkopesha mlalamikaji Tsh. 1,000,000/= lakini alilipwa kiasi cha Tshs. 18,000,000/= (Milioni Kumi na Nane) kama deni la mkopo na riba.

Mkopeshaji huyu amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 17,000,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 10,800,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Tshs. 6,200,000/=.

Vilevile **Mkopeshaji wa pili** naye akiwa mtumishi wa kampuni ya ukopeshaji **MALICHA MICROCREDIT CO LTD** yeye binafsi alimkopesha mlalamikaji Tsh. 4,000,000/= ambapo wakati wa malipo alilipwa kiasi cha Tshs. 12,000,000/= (Milioni Kumi na mbili).

Mkopeshaji wa pili amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 8,000,000/= alichukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 3,700,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Tshs. 4,300,000/=.

Mkopeshaji wa tatu akiwa mkurugenzi wa kampuni ya KYANYARI CO. LTD iliyokuwa inayojishughulisha na utoaji wa mikopo kupitia kampuni hiyo alimkopesha malalamikaji Tsh. 2,000,000/= lakini alilipwa kiasi cha Tshs. 22,000,000/= (Milioni ishirini na mbili) kama deni la mkopo na riba.

Mkopeshaji huyu amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 20,000,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 3,000,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Tshs. 17,000,000/=

Hivyo fedha za Mwalimu huyo Mstaafu zilizochukuliwa isivyostahili ni Tshs. 45,000,000/= (Milioni arobaini na tano) ambapo tayari kiasi cha Tshs. 17,500,000/= zimesharejeshwa na nyingine zinaendelea kurejeshwa.

2. Mstaafu wa pili.

Huyu ni mstaafu wa idara ya afya. Mnamo mwaka 2018 alikopa kiasi cha Tshs. 6,000,000/= toka kampuni ya **NYAKIHA CO. LTD**. kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo baada ya kupata mafao ya kustaafu.

Mtuhumiwa wa nne ambaye ni mmiliki wa kampuni ya **NYAKIHA CO. LTD** kupitia kampuni yake alimkopesha mstaafu huyo kiasi cha Tshs. 6,000,000/= lakini alilipwa kiasi cha Tshs. 26,000,000/= (Milioni ishirini na sita) kama deni la mkopo na riba.

Baada ya miezi kadhaa mstaafu alilipwa mafao yake, alipoenda kulipa deni lake kwa mkopeshaji kiasi cha Tshs. 6,000,000/= alitakiwa kulipa kiasi cha Sh. 26,000,000/= kama deni la mkopo na riba.

Mmiliki wa kampuni hii amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 20,000,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 11,000,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Tshs. 9,000,000/=.

Hivyo fedha za Mstaafu huyo zilizochukuliwa isivyostahili ni Tshs. 20,000,000/= (Milioni ishirini) ambapo tayari kiasi cha Tshs. 17,500,000/= zimesharejeshwa na nyingine zinaendelea kurejeshwa.

3. Mstaafu wa tatu.

Huyu ni mwalimu mstaafu alikopa kiasi cha Tshs. 3,000,000/= kutoka kwa watu watatu tofauti kwa makubaliano ya kurejesha fedha hizo baada ya kupata mafao ya kustaafu kama ifuatavyo:-

Mkopeshaji wa kwanza alimkopesha mstaafu kiasi cha Tshs. 2,000,000/= lakini wa alilipwa kiasi cha Tshs. 10,000,000/= (Milioni kumi) kama deni la mkopo na riba.

Katika makubaliano yaliyofanyika kupitia ofisi ya **OCD** Kahama mtuhumiwa alikubali kurejesha kiasi cha Tshs. 6,500,000/= alichochukua isivyo halali na alimrejeshea mlalamikaji kiasi cha Tshs. 4,000,000/= mnamo tarehe 26/06/2020. Aidha kiasi kilichobaki cha Tshs. 2,500,000/= mtuhumiwa alikirejesha kupitia ofisi hii mnamo tarehe 10/07/2020.

Mkopeshaji wa pili ambaye ni mwalimu wa shule ya sekondari Ibisabageni ambapo alimkopesha mlalamikaji kiasi cha Tshs. 1,000,000/= (milion moja) alilipwa kiasi cha Tshs. 10,000,000/= (Milioni kumi) kama deni la mkopo na riba.

Mkopeshaji amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 9,000,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 1,000,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Sh. 8,000,000/=

Vilevile Mstaafu huyu aliwahi kudhurumiwa kiasi cha Sh. 12,200,000/= na alidhurumiwa na mkuu wa shule ya Sekondari KAHUMULO.

Mkopeshaji amekubali kurejesha kiasi cha Tshs. 12,200,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha kiasi cha Tshs. 500,000/=. Hivyo bado anadaiwa kiasi cha Tshs. 11,700,000/=.

Hivyo fedha za Mwalimu huyo mstaafu zilizochukuliwa isivyostahili ni Tshs. 27,700,000/= (Milioni ishirini na saba na laki saba) ambapo kiasi tayari kiasi cha Tshs. 8,000,000/= zimesharejeshwa na nyingine zinaendelea kurejeshwa

4. Mstaafu wa nne.
Huyu ni mwalimu mstaafu alikopa kiasi cha Tshs.7,450,000/= kutoka kwa watu watatu tofauti kama ifuatavyo:-

Mkopeshaji wa kwanza alimkopesha Mwalimu mstaafu kiasi cha Sh. 4,450,000/= lakini alilipwa kiasi cha Tshs. 8,268,000/= (Milioni nane laki mbili na sitini na nane elfu) kama deni la mkopo na riba.

Mkopeshaji alikubali kurejesha kiasi cha Tshs. 3,818,000/= alichochukua isivyo halali na tayari amesharejesha fedha hizo tarehe 16/06/2020.

Mkopeshaji wa pili ambaye ni mtumishi wa kampuni ya NASSERO INVESTIMENT CO. LTD alichukua kiasi cha Tshs. 1,850,000/= kutoka kwa mwalimu mstaafu isivyo halali. Aidha Mkopeshaji alirejesha kiasi chote tajwa.

Aidha **Mkopeshaji wa tatu** anatafutwa ili aweze kurejesha kiasi cha Tshs. 7,000,000/= alizochukua isivyo halali.

Hivyo fedha za Mwalimu mstaafu zilizochukuliwa isivyostahili ni Tshs.12,668,000/= (Milioni kumi na mbili laki sita sitini na nane) ambapo tayari kiasi cha Tshs. 4,000,000/= zimesharejeshwa.

5. Mstaafu wa tano.
Huyu mkazi wa Shinyanga mjini ambapo alidhurumiwa kiasi cha Tshs. 3,100,000 na mkopeshaji wa mikopo umiza katika biashara zao walizofanya hivyo kupitia ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa shinyanga mkopeshaji amerejesha kiasi chote tajwa.

Kwa upande wa Dawati la Kuzuia Rushwa, TAKUKURU mkoa wa Shinyanga imeendelea kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo inayopewa fedha za Serikali na ufadhili wa wadau wa maendeleo. TAKUKURU Shinyanga ilifuatilia matumizi ya fedha za miradi **miwili ya Afya na mradi mmoja wa Elimu** yenye thamani ya jumla ya **Sh. 411, 000, 00/=** ambapo uchambuzi wa kina katika matumizi ya fedha hizi unaendelea na pale itakapobainika kuna ubadhilifu sheria itachukua mkondo wake.

Kwa upande Dawati la Uchunguzi, TAKUKURU mkoa wa Shinyanga kwa kipindi cha robo ya tatu Aprili–Juni cha mwaka wa fedha 2019/2020 tumepokea taarifa 76 ambazo baadhi uchunguzi umekamilika na nyingine bado unaendelea.

Kwa mujibu wa taarifa tulizopokea idara zilizolalamikiwa ni kama ifuatavyo: Mikopo umiza(12), Serikali za Mitaa (12), Ushirika (8), Elimu (6), Taasisi za fedha (6), Afya (5), Mahakam (5), Ardhi (5), Siasa (4), Polisi (4), Ujenzi (3), Madini (2), Kilimo(2), na maji (2).

Kesi zinazoendelea mahakamani ni 30 kati ya hizo kesi mpya ni (5) na kesi mbili iliyoamuliwa kwa kupata ushindi mahakamani. Mchanganuo wa kesi zinazoendelea mahakamani kisekta ni kama ifuatavyo; serikali za mitaa kesi (13), Elimu kesi (7), Idara ya Afya kesi (3), Uhamiaji kesi (1), NIDA (1), Usafirishaji (1), Tasaf (1) Michezo (1), Taasisi za fedha (1) na mahakama (1)

Kwa upande wa Dawati la Elimu kwa Umma, Taasisi imeendelea na jukumu lake la kuelimisha umma huku ikitoa kipaumbele kuelimisha wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kufanya kazi zifuatazo;

NA	KAZI ZILIZOFANYIKA	IDADI
1.	Semina.	3
2.	Mikutano ya hadhara.	29
3.	Uimarishaji wa klabu.	31

4.	Habari/Makala.	01
5.	Maonesho.	01
6.	Mikutano na vyombo vya habari.	01
Jumla ya wananchi 24,045 walielimishwa.		

MIKAKATI YA UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU MKOA WA SHINYANGA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA, 2020.

Mkakati mkubwa kwa kipindi hiki ni kuendelea kutoa elimu ya rushwa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. Elimu hiyo itatolewa kwa wananchi wote kwa maana ya wapiga kura na wale watakaogombea nafasi mbalimbali elimu inayotolewa itahusu mamo yafuatayo:-

- Makosa ya rushwa katika chaguzi za kisiasa.
- Sheria ya gharama za uchaguzi kama zilivyoainishwa na sheria ya gharama za uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010.
- Makosa yaliyopo kwenye sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Hapa nitoe rai kwa wagombea wote watakaochaguliwa na vyama vyote vya siasa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kuwa makini na mienendo yao na kuhakikisha kwa namna yoyote hawajihusishi na vitendo vyovyote kinyume na sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007, Sheria ya gharama za uchaguzi kama zilivyoainishwa na sheria ya gharama za uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010 pamoja na Sheria ya uchaguzi Namba 1 ya mwaka 1985 na marekebisho yake.

WITO

Kwa kupitia mkutano huu naomba nitoe wito kwa wananchi wote wa mkoa wa Shinyanga kutokubali kununuliwa na wanasiasa pia kuwataka waendelee kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kama ambavyo wamekuwa wakifanya ili kuhakikisha kuwa tunaondoa kero ya rushwa katika Mkoa wetu hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandishi wote wa habari wa mkoa wa Shinyanga kwa kushiriki kwenu katika mapambano dhidi ya rushwa.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Imetolewa na Hussein M. Mussa Mkuu wa TAKUKURU (M) Shinyanga.